



## Watafufuliwa watu siku ya Kiyama wakiwa peku, uchi, hawajatahiriwa

Kutoka kwa Aisha radhi za Allah ziwe juu yake- amesema: Nilimsikia Mtume rehema na amani ziwe juu yake- akisema: "Watafufuliwa watu siku ya Kiyama wakiwa peku, uchi, hawajatahiriwa" Nikasema: Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, wanawake na wanaume wote pamoja, kila mmoja anamtazama mwenzake? Akasema rehema na amani ziwe juu yake: "Ewe Aisha, jambo litakuwa kubwa mno, kuliko hata mtu kushughulika kumtazama mwenzake".

[Sahih] [Wamekubaliana Bukhaariy na Muslim]

Amesimulia Mtume rehema na amani ziwe juu yake baadhi ya yale yatakayokuwa siku ya Kiyama, na kwamba watakusanya watu baada ya kufufuliwa kutoka makaburini mwao kwa ajili ya hesabu, na hali yao ni kwamba watakuwa miguu peku bila viatu, miili yao ikiwa uchi bila nguo wala kizuizi, na wakiwa hawajatahiriwa kama siku waliyozaliwa na mama zao, aliposikia mama wa Waumini Aisha radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake akasema kwa kustaajabu: Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, wanawake na wanaume wote pamoja kila mmoja akimtazama mwenzake?! Mtume rehema na amani ziwe juu yake akambainishia: Kwa jambo la kisimamo na kukusanya baada ya kufufuliwa kutoka katika kifo lina misukosuko kiasi kwamba watu macho yao hayatojali kutazama utupu.

<https://sunnah.global/hadeeth/sw/show/5460>

